JINA: …… NAMBARI: ……..

SAHIHI: …….. SHULE: ……

101/2
KISWAHILI
KARATASI YA 2
LUGHA
JULAI / AGOSTI 2011
MUDA: SAA 1 ¾

MTIHANI WA MUUNGANO WA WILAYA ZA NANDI KUSINI, NANDI MASHARIKI NA TINDERET

MAAGIZO

(a) *Jibu Maswali yote.*

(b) *Andika majibu yako katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE

SWALI	UPEO	ALAMA
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
JUMLA	**80**	

© 2011 Mtihani wa Muungano wa Wilaya za Nandi Kusini, Nandi Mashariki na Tinderet

1. **UFAHAMU:**
Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali yafuatayo.

Maisha ya binadamu yamepitia katika hatua mbalimbali katika karne kadha zilizopita. Uzalishaji wa kawi, kwa mfano, umeshuhudia mageuko makubwa kuanzia enzi za zama kongwe za mawe ambapo mawe yalikuwa nyenzo kuu ya uzalishaji wa kawi na nishati. Mojawapo wa nyanja ambazo zimepiga misamba mikubwa ya maendeleo ni ile ya mawasiliano. Maelezo ya jinsi usafiri wa zamani ulivyotegemea uwezo wa binadamu kutembea kutoka sehemu moja hadi nyingine yanasikika kama kadhia za paukwa pakawa.

Karne tunayoishi ni karne ambayo huenda ikashuhudia maendeleo yasiyokadirika katika nyanja hii. Kwa sasa hivi, tarakilish imekuwa nyenzo kuu ya mabadiliko hayo kutokana na nafasi muhimu inayochukua katika maisha yetu. Tangu azali tumesikia msemo kuwa 'maarifa ni uwezo.' Ukweli wa msemo huu unadhihirika bayana tuangaliapo nafasi ya tarakilishi kama jira ya teknolojia ya habari na mawasiliano au teknohama.

Maendeleo makubwa ya wavuti au mdahalishi katika ulimwengu wa sasa yanasahilisha mawasiliano ya jamaa, ndugu na watu wanaoishi maeneo mbalimbali. Kasi ya uenezaji wa maarifa ukekuwa ya juu sana. Mikahawa ya mdahalishi au vituo vya bwakameme (*cybercafés*) vimeenea kila mahali. Inahitaji muda mfupi kusakura kwenye mdahalishi na kupata maarifa unayoyatamani. Kwa njia hii mtumiaji anapata maarifa muhimu kwa bei nafuu na kwa njia nyepesi na rahisi kuliko kulazimika kubukua mabuku ya kila aina kupata taarifa sawa na hizo.

Ili kuweza kuifaidi enzi hii ya teknohama pana haja kubwa ya mataifa yetu kuwekeza katika wanja huu. Serikali zetu zinapaswa kutambua kuwa jamii kutoijua taaluma ya tarakilishi, angaa ile ya kimsingi, ni kama kutojua kusoma katika enzi zilizopita. Kadiri wakati unavyosonga ndivyo ambavyo tarakilishi inavyochukua nafasi muhimu katika maisha yetu. Katika msingi huu basi lazima ziwepo juhudi za kuyaeneza maarifa muhimu kuhusu matumizi yake. Inahalisi kutambua kuwa mtaka cha mvunguni sharti ainame. Ikiwa tunataka jamii yetu iyafaidi matunda ya teknolojia ya leo basi hatuna budi kuwa tayari kuwekeza ipasavyo.

Uwekezaji huo unaenda sambamba na juhudi za kuhakikisha elimu inayohusiana na masuala ya tarakilishi inasambazwa nchini. Elimu hii ndiyo maarifa ambayo yatakuwa nguzo ya kimsingi ya maendeleo ya nchi siku za usoni. Ni muhimu hata hivyo kutoa tahadhari hapa. Katika jamii nyingi huwepo watu ambao kila panapokuwa na mvuvumko fulani hupenda kuitumia hali hiyo kujinufaisha. Huweza kufanya hivi kwa kuanzisha vituo vya kufundishia maarifa dufu ya tarakilishi nia yao ikiwa ni kufaidika kutokana na karo ghali wanazotoza. Licha ya kuwa tunasisitiza umuhimu wa kuwepo na kusambazwa kwa elimu ya tarakilishi, pana haja ya kuwapo na viwango. Lazima serikali ihakikishe kuwa pana viwango vinavyodumishwa. Hii itazuia uwezekano wa kuanzishwa kwa shule ambazo lengo lake la kimsingi sio kuyaendeleza maarifa ya jamii bali kuijaza mifuko ya wachache waliozugwa na shauku ya utajiri.

Maisha ya kesho yatadhibitiwa kwa kiasi kikubwa na tarakilishi. Leo hii hata biashara inaendelezwa kwa mfumo huu. Huu ndio msingi wa biasharalishi au biashara ya elektroniki (*e-commerce*) ambayo imeanza kushika kasi ulimwenguni. Biashara ya aina hii inayawezesha makampuni mengi kuwafikia wateja wake popote walipo ulimwenguni. Umbali wa kijiografia sio kikwazo tena kwa kuwa biashara ya aina hii haitegemei makutano ya ana kwa ana kati ya mteja na mwuzaji.

Lazima ziwepo juhudi nyingi sio tu za kusambaza na kuineza taaluma ya tarakilishi bali pia kuhakikisha kuwa taasisi nyingi zimetarakilishwa ili kwenda sambamba na wakati. Wakati wa kulundika majalada ofisini kama maghala umepita. Hii ni enzi ya teknohama.

© 2011 Mtihani wa Muungano wa Wilaya za Nandi Kusini, Nandi Mashariki na Tinderet

MASWALI

(a) Ni kwa jinsi gani mawasiliano imepiga misamba mikubwa ya maendeleo. (alama 2)

……

……

(b) Mdahalishi umesahilisha mawasiliano, fafanua kauli hii kulingana na muktadha. (alama 2)

……

……

(c) Kwa mujibu wa taarifa nchi zinazoendelea zinaweza kufaidi enzi hii ya teknohama vipi? (alama 4)

……

……

……

……

(d) Kando na sekta ya elimu, ni sekta gani nyingine ambayo mwandishi anapendekeza kuwa imefaidika na enzi hii ya teknohama. (alama 1)

……

(e) Pashau ya wachache waliozugwa na shauku ya utajiri wanaweza kudhibitiwa vipi na serikali? (alama 2)

……

……

(f) Eleza maana ya: (alama 4)

(a) Tangu azali: ……

(b) Zimepiga misamba mikubwa: ……

(c) Mvuvumko: ……

(d) Maarifa dufu: ……..

2. **UFUPISHO**

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Mwana wa Adamu ni kiumbe cha ajabu! Ni kiumbe kilichopewa uwezo wa kuhodhi na kumiliki kila kitu; kiumbe kilichopewa akili na maarifa fuvu tele ili kuratibu shughuli na urari wa mambo; kiumbe kichopewa uwezo wa kuwasiliana na kutimia sauti nasibu ili kuwa na urari na muwala; kiumbe kilichopewa uwezo wa kufaidi viumbe wengine kwa njia mbalimbali na jumla jamala; hichi ndicho kiumbe kilichopewa idhini maalumu ya kuzaana na kujaza dunia. Huyu ndiye mwana wa mama Hawa ambaye sasa amegeuka ndovu kumla mwanawe.

Kwa sababu ya bongo alizonazo, binadamu ana uwezo wa kutumia teknolojia kwa manufaa yake na ithibati zipo tele. Binadamu ametumia nyambizi kuzuru chini ya bahari; amefika mwezini; amevumbua mangala; amevumbua uyoka; amevumbua tarakilishi na sasa shughuli zake ni za kutandaridhi. Mwenyewe yuasema kuwa dunia yake amekuwa kitongoji katika muumano huu.

© 2011 Mtihani wa Muungano wa Wilaya za Nandi Kusini, Nandi Mashariki na Tinderet

Chambacho wavyele, akili nyingi huondoa maarifa. Binadamu amekuwa dubwana linalojenga kushoto na kubomoa kulia na tuna sababu ya kulisoza dubwana hili kidole. Rabana ndiye msanii asiye mfanowe kwani aliisawiri dunia kwa kila lililo jema kwa siku sita mtawala na kumpa binadamu mazingira murua. Rubuka akaona yote yalikuwa mema na mazuri; akamwambia binadamu, "Haya, twende kazi!"

Viwanda vya binadamu vinatiririsha maji-taka ovyo hadi mitoni, maziwani na baharini na matokeo yamekuwa ni vifo vya viumbe vya majini kama samaki ambavyo ni urithi aliopewa na Muumba. Hakuna kiumbe kinchoweza kustahimili maisha bila maji safi. Maji yote sasa yametiwa sumu na binadamu kwa sababu ya 'maendeleo' yake. Joshi kutoka katika viwanda vivyo hivyo nalo limehasiri ukanda wa ozoni ambao sasa umeruhusu jua kutuhasiri kwa joto kali mno. Siku hizi inasemekana kuwa kuna mvua ya asidi inayonyesha katika baadhi ya sehemu za dunia na kuleta madhara makubwa. Labda hata mabahari yamekasirika kwa sababu hivi majuzi katika kile kilichoitwa 'tsunami', bahari lilihamia nchi kavu na kusomba maelfu ya binadamu na kuwameza wazima wazima. Vimbunga navyo vimetokea kwa wingi. Wataalamu wanasema kuwa viwango vya miyeyuko vitazidi kwa sababu ya joto na kiwango cha maji kitazidi pia. Binadamu atatorokea wapi?

Idadi ya binadamu imezidi hadi kiasi asichoweza kukishughulikia kwa sababu anaijaza kiholela kwa sababu anadai kuwa aliruhusiwa kuijaza. Hii ni imani potovu. Anasahau kuwa ulipewa ubongo wa kuwaza na kuwazua kabla ya kufanya chochote. Dhiki, maradhi na ufukara zimehamia kwa binadamu na kumtia kiwewe.

Binadamu amefyeka misitu kwa kutaka makao, mashamba, mbao, makaa, ujenzi wa nyumba na barabara na mahitaji mengine mengi. Wanyama wamefurushwa na wengi kuangamia kwa sababu ya ukosefu wa chakula na wengine kushindwa kuhimili mabadiliko katika mazingira. Chemichemi za maji zimekauka nalo jangwa limeanza kutuzuru kwa kasi inayotisha. Kazi ya binadamu imekuwa ya kusukia kamba motoni. Itambidi aanze kujenga kwa matofali ya barafu!

(a) Kwa nini Mwana wa Adamu ni kiumbe cha ajabu? (Tumia maneno 40 – 50). (alama 4)

Matayarisho (Mtiririko alama 1)

……

……

……

……

Jibu

……

……

……

……

……

(b) Fupisha aya tatu za mwisho ukitumia maneno 85 – 90. (alama 8)

Matayarisho (Mtiririko alama 2)

……

……

……

© 2011 Mtihani wa Muungano wa Wilaya za Nandi Kusini, Nandi Mashariki na Tinderet

……

……

……

……

Jibu

……

……

……

……

……

……

……

……

3. **MATUMIZI LA LUGHA**

(a) Tunga sentensi moja ukitumia nomino ya kitenzi jina. (alama 2)

……

……

(b) Tofautisha sauti zifuatazo /g/ /gh/ /ng'/ na /kh/ (alama 2)

……

……

(c) Andika sentensi ifuatayo kwa umoja. Mbavu zao nyingi zilivunjika. (alama 2)

……

(d) Unganisha sentensi zifuatazo iwe sentensi moja. (alama 2)

Hizi ni bidhaa zangu. Nilizitoa bidhaa hizi Bungoma. Bidhaa hizi ni za kuuzwa.

……

(e) Eleza matumizi ya KI katika sentensi ifuatayo:

Kitoto kimekuwa kikila kikiimba kikasuku. (alama 3)

……

……

(f) Tunga sentensi yenye viungo vifuatavyo vya sarufi. (alama 3)

(i) Shina la kitenzi cha silabi moja.

(ii) Mnyambuliko wa kitenzi kauli ya kufanyia.

(iii) Kikanushi.

(iv) Kiwakilishi cha wakati uliopita.

© 2011 Mtihani wa Muungano wa Wilaya za Nandi Kusini, Nandi Mashariki na Tinderet

(v) Mtendwa katika nafsi ya tatu.

(vi) Kiima katika nafsi ya pili.

……

……

(g) Akifisha kifungu kifuatacho. (alama 3)

Kweli wanafunzi hao walifanya bidii karibu wote walipata kati ya a na c wakapewa zawadi km saa za ukuta, miavuli ya tbc tarakilishi na hata simu tamba.

……

……

(h) Yakinisha katika umoja. Nguzi zisingekatika zisingepotea, (alama 2)

……

(i) Tunga sentensi moja moja kuonyesha tofauti ya vitate vifuatavyo. (alama 2)

(i) Dhiraa: ……

(ii) Dira: ……

(j) Onyesha shamirisho kipozi na kitondo katika sentensi.

Fuad alivunja mlango wa nyumba yake. (alama 2)

…….

(k) Onyesha kishazi huru na kishazi tegemezi katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

Pindi kipenga kilipopulizwa wanafunzi walipiga foleni.

……

(l) Andika sentensi ifuatayo ukitumia kirejeleo cha ngeli mwafaka. (alama 2)

Milango yote ilijifunga ovyo na ikafunguliwa.

……

(m) Tambua kwa kupigia mstari aina za vivai. (alama 2)

(i) Miti ilipandwa kando yam to.

(ii) Kuimba huko kunaudhi.

(n) Tunga sentensi moja kubainisha matumizi ya vihusishi vya wakati, vihusishi vya a-, na vihusishi vya hali. (alama 3)

……

……

(o) Huku ukitoa mifano mwafaka eleza matumizi mawili ya parandesi. (alama 2)

……

……

© 2011 Mtihani wa Muungano wa Wilaya za Nandi Kusini, Nandi Mashariki na Tinderet

(p) Changanua kwa kuchorea matawi. (alama 6)

Mwanafunzi aliyepita mtihani alituzwa na mgeni wa heshima.

……

……

……

……

……

……

4. **ISIMU JAMII**

(a) Fafanua changamoto zozote tano zinazokumba lugha ya Kiswahili nchini Kenya. (alama 5)

……

……

……

……

……

……

……

(b) Eleza sababu tano zinazochangia kuenea kwa lugha ya Kiswahili. (alama 5)

……

……

……

……

……

……

© 2011 Mtihani wa Muungano wa Wilaya za Nandi Kusini, Nandi Mashariki na Tinderet